**Chanjo kwa watoto wako wa miaka 11-12:**

Rx

- √ Tdap
- √ HPV
- √ Meningococcal

## VIRUSI VYA PAPILOMA KWA BINADAMU (HPV)

**HPV ni virusi vya kawaida ambavyo vinaweza kusababisha saratani.**
***Chanjo ya HPV ni kinga dhidi ya saratani na wewe ndiwe ufunguo.***

Chanjo ya HPV huzuia maambukizi kutoka kwenye aina za HPV zenye madhara sana. Chanjo ni salama na inafanya kazi na inapendekezwa kwa wavulana na wasichana kuanzia umri wa miaka 11 au 12.

Chanjo ya HPV hulinda dhidi ya aina maarufu sana za virusi vya papiloma kwa binadamu, ambavyo vinawajibikia asilimia 90 ya saratani zote za kizazi na madutu ya uzazi. Wavulana na wasichana wanapaswa kupata chanjo kamilifu kwa ajili ya kinga kamili. Chanjo inafanya kazi vizuri wakati inapopewa katika ujana wa mapema na kuruhusu muda wa kingamwili kukua, kumaanisha ulinzi bora mtoto wako anapokua zaidi.




**Zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu chanjo leo. Pata chanjo kwa maisha bora!**

**CHANJO YA HPV NDIO UFUNGUO**

IDPH

Ikiwa una maswali, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wako wa afya au Iowa Department of Public Health kwa nambari

**1-800-831-6293**

**http://idph.iowa.gov/ImmTB/Immunization**

**KWA MAELEZO ZAIDI KUHUSU CHANJO NA MAGONJWA, TAFADHALI TEMBELEA:**

**www.immunize.org • www.cdc.gov/vaccines/teens**
**www.vaccine.chop.edu • www.aap.org**

Januari 2017

# UNAWEZA KUZUIA SARATANI

**CHANJO YA HPV NDIO UFUNGUO**

IDPH

Wazazi na wataalamu wa huduma ya afya ni ***muhimu*** kwa kulinda vijana dhidi ya saratani za HPV.

# HPV NI NINI?

HPV ni virusi ambavyo takribani kila mtu ataambukizwa wakati fulani maishani mwake. HPV husambazwa kupitia ngono na inaweza kusambazwa hata wakati mtu aliyeambukizwa hana ishara wala dalili. Mara nyingi, maambukizi ya HPV hutoweka yenyewe na watu walioambukizwa virusi hawakuwahi kujua kuwa walikuwa navyo. Hata hivyo, wakati HPV haijatoweka, inaweza kusababisha matatizo ya afya kama vile madutu ya uzazi na saratani. Saratani mara nyingi huchukua miaka mingi kukua baada ya mtu kuambukizwa HPV.

HPV inaweza kuwa na madhara mengi sana mabaya kwa wanaume na wanawake zikiwemo:

- **SARATANI YA KIZAZI**
- **SARATANI YA TUPU YA KIKE**
- **SARATANI YA UKE**
- **SARATANI YA SEHEMU YA NYUMA**
- **SARATANI YA UUME**
- **SARATANI YA KOO** *(saratani nyuma ya koo, ikiwemo sehemu ya ulimi na mafindo)*
- **MADUTU YA UZAZI**
- **PAPILLOMATOSIS YA UPUMUAJI WA KUJIRUDIA (RRP)** *(hali isiyo ya kawaida ambapo madutu hukua katika koo)*

Takribani Wamarekani milioni 79 kwa sasa wameambukizwa HPV na watu milioni 14 huambukizwa upya kila mwaka. Takribani saratani 33,000 zinazohusishwa na HPV hutokea kila mwaka Marekani, zikiwemo saratani 12,600 zinazohusishwa na HPV kwa wanaume.

American Cancer Society (ACS) inaonyesha visa vipya 12,000 vya saratani ya kizazi ya ndani zaidi vitatokea Marekani na karibu wanawake 4,000 wataaga dunia kutokana na ugonjwa huu kila mwaka. Duniani kote, saratani ya kizazi ndiyo saratani ya pili maarufu zaidi kwa wanawake na inakadiriwa kusababisha zaidi ya visa vipya 470,000 na vifo 233,000 kila mwaka.

# KINGA YA HPV

Chanjo ya HPV ni kinga bora dhidi ya aina maarufu zaidi za virusi vya papiloma kwa binadamu. Chanjo hutoa manufaa bora zaidi ya afya kwa watu wanaokamilisha mfululizo kabla ya hatari yoyote ya HPV. Wataalamu wa afya wanapendekeza chanjo ya mara kwa mara ya wavulana na wasichana wenye umri wa miaka 11 au 12 kwa chanjo waliyokosa kwa vijana na mabarubaru.

## UNAHITAJI DOZI NGAPI NA KWA RATIBA GANI?

Chanjo ya HPV ina mfuatano wa dozi mbili au tatu kwa kipindi cha miezi sita na zinaweza kutolewa kwa wakati mmoja kama chanjo nyingine. Mfuatano wa chanjo ya HPV uliokamilika ni muhimu ili kutoa kinga kamilifu. Chanjo hufanya kazi vizuri na kutoa mkabiliano wa kinga ya juu zaidi kwa vijana wachanga (miaka 11-12) kuliko inavyofanya kwa mabarubaru na vijana wakubwa.

## JE, CHANJO YA HPV NI SALAMA?

Chanjo ya HPV ni salama na inafanya kazi. Chanjo ya kwanza ya HPV ilipatikana mwaka wa 2006 na tangu wakati huo, zaidi ya dozi milioni 40 za chanjo zimetolewa. Hakujawa na matatizo mabaya ya usalama yanayohusishwa na chanjo ya HPV.

Hata hivyo, kama dawa yoyote, chanjo zinaweza kusababisha athari nyingine. Athari nyingine maarufu sana kutoka kwenye chanjo ya HPV ni ndogo na ni pamoja na maumivu au uvimbe mahali chanjo ilipotolewa, homa au maumivu ya kichwa ya kiwango cha chini. Dalili ndogo kama hizo ni za kawaida na zinapaswa kutarajiwa mwili unapojenga kinga. Mikabiliano mibaya ni nadra sana.

Chanjo hufanywa kwa kiwango cha juu zaidi cha usalama. Marekani ina chanjo salama na inayofanya kazi vizuri zaidi katika historia. Miaka ya majaribio inahitajika kisheria kabla ya chanjo kupewa leseni. Mara tu inapoanza kutumika, chanjo huendelea kufuatiliwa kwa ajili ya usalama na utendakazi. Mtu yeyote anayepata chanjo anapaswa kufahamu kikamilifu kuhusu manufaa na hatari. Maswali au masuala yoyote yanapaswa kujadiliwa na mtoa huduma wako wa afya.

## JE, KUNA USAIDIZI WA GHARAMA YA CHANJO?

Angalia ili uone ikiwa bima yako ya afya inashughulikia chanjo ya HPV. Ikiwa mtoto wako hana bima ya afya au hana bima inayogharimia chanjo, mwulize mtoa huduma wako wa afya kuhusu mpango wa Vaccines for Children (VFC). Mpango wa CFC unatoa chanjo kwa watoto wanaostahiki kutoka wakati wa kuzaliwa hadi miaka 18.

## REKODI YA CHANJO YA MTOTO WAKO

Ni muhimu kuhifadhi rekodi za chanjo katika eneo salama. Thibitisho la chanjo linaweza kuhitajika maishani mote. Iowa Department of Public Health haidumishi rekodi za chanjo za karatasi za historia. Hata hivyo, rekodi za chanjo zinaweza kuwekwa katika hifadhidata ya elektroniki ya kudumu ya jimbo zima inayoitwa Iowa's Immunization Registry Information System (IRIS) (Mfumo wa Maelezo ya Usajili wa Chanjo wa Iowa).

IRIS ina kipengele cha kufikia rekodi za umma ambacho huruhusu wazazi au watu wazima kutafuta rekodi za chanjo zao binafsi au za watoto wao kwenye https://iris.iowa.gov. Ikiwa rekodi hazipatikani, mwombe mtoa huduma wako wa afya aweke rekodi yako ya chanjo kwenye IRIS.



**HPV HUSABABISHA SARATANI kwa Wamarekani 33,000 kila mwaka —**

**yaani mtu 1 takribani kila baada ya dakika 16.**